

1 K₂

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

Anuani ya Simu: ELIMU DAR ES
SALAAM.
Simu: 2120402, 2120413,
2120403/4/ 5/7/8/9
Telex: 42741 Elimu Tz.
Fax: 2113271 Elimu Tz
Unapojibu tafadhali taja:



S.L.P 9121,
DAR ES SALAAM

Kumb. Na. ED/0KE/NYE/Vol. I/20

Tarehe: 03/08/2012

Makatibu Tawala wa Mikoa
Makatibu Tawala wa Wilaya
Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Kanda
Wakaguzi Wakuu wa Shule wa Wilaya
Wakuu wa Vyu vya Ualimu
Wakuu wa Shule za Sekondari Walimu
Wakuu wa Shule za Msingi
TANZANIA BARA.

**WARAKA WA ELIMU NA. 4 WA MWAKA 2012 WANAFUNZI
KUFUKUZWA SHULE/CHUO KABLA YA MTIHANI WA TAIFA
KUFANYIKA**

Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 na Rekebisho lake Sura ya 353 Kifungu Na. 35(3) ya mwaka 2002, inaeleza kuwa kila mwanafunzi akijiandikisha shule hana budi kuhudhuria na kumaliza shule katika ngazi husika. Aidha, mipango yote ya Elimu: Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi [MMEM] na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari [MMES], inasisitiza wanafunzi kuandikishwa, kuhudhuria na kumaliza masomo yao katika ngazi husika.

Pamoja na kwamba ni lazima wanafunzi walioandikishwa kuhudhuria na kumaliza masomo katika ngazi husika ya elimu, baadhi ya shule/vyuo wamekuwa na utamaduni wa kuwasimamisha au kuwafukuza shule/chuo wanafunzi wakati mitihani inapokaribia kutokana na makosa mbalimbali ya utovu wa nidhamu. Kamati au Bodi za Shule/Chuo hutoa adhabu ya kuwafukuza wanafunzi hao shule/chuo wakati wanakaribia kufanya mitihani yao ya mwisho kwa ajili ya kuhitimu ngazi husika ya masomo.

Matatizo mengi ya utovu wa nidhamu yangeweza kushughulikiwa mapema na shule au chuo badala ya kusubiri wakati mitihani inapokaribia. Kitendo cha kufukuza wanafunzi wakati mitihani inapokaribia kinasababisha usumbufu mkubwa kwa wanafunzi wenyewe na wazazi/walezi wao. Vilevile, hali hiyo inaisababishia Serikali hasara kubwa ya gharama ya maandalizi yote ya mitihani ya Taifa.

Kutokana na hali hiyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inaagiza kuwa mwanafunzi/mwanachuo yeyote asipewe adhabu ya kufukuzwa shule/chuo akiwa katika mwaka wa maandalizi ya kufanya mitihani ya Taifa ya kuhitimu darasa la VII, Kidato cha IV na kidato cha VI. Badala yake adhabu mbadala itolewe kwa wanafunzi ili kuondoa usumbufu kwa wanafunzi wenyewe na wazazi au walezi wao. **Makosa ya jinai tu**, ndiyo Kamati/Bodi italazimika kumfukuza shule/chuo mwanafunzi/mwanachuo.

Endapo Kamati au Bodi italazimika kumsimamisha masomo mwanafunzi wakati au ndani ya kipindi cha mitihani, mwanafunzi huyo asinyimwe kufanya mitihani na badala yake aruhusiwe kufanya mitihani hiyo katika kituo chake akiwa nje ya utaratibu wa shule.

Ni jukumu la uongozi wa shule na walimu wote kujua mienendo na tabia za wanafunzi mapema ili kuepusha tatizo la kuwafukuza shule/chuo muda mfupi kabla ya mitihani wa kitaifa kufanyika.

Waraka huu, unafuta mwongozo na nyaraka zote za nyuma kuhusu wanafunzi kufukuzwa shule/chuo kabla ya mitihani wa Taifa kufanyika na unanza kutumika mara moja.



M. M. Wassena

KAIMU KAMISHNA WA ELIMU

Nakala: Katibu Mkuu,
OWM TAMISEMI
S.L.P. 1923,
DODOMA

Mkurugenzi,
Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima,
S.L.P. 20679
DAR ES SALAAM

Katibu Mtendaji,
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
DAR ES SALAAM